**أحوالُ الفرجِ والشدةِ**

**"Hali za faraja na shida"**

**Imefasiriwa na**

**profesa/ Ayman Alasar**

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, anayesema katika Qur'ani Tukufu:

"وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِنْ شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ"

**"Na alipo tangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru nitakuzidishieni",** na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu msalie, mpe salamu na umbariki yeye, Familia yake, Masahaba zake, na Kila atakayewafuata kwa wema mpaka Siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu

**Amma bado,,,**

Ni Sunna ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika viumbe vyake kuyajaalia maisha hubadilishwa baina ya shida na faraja, dhiki na wasaa, na huzuni na furaha, basi watu wa imani ndio ambao katika hali zote hizi wawe kati ya subira na shukrani, ambapo Mtume wetu (S.A.W) anasema:

"عَجَبًا لِأَمْرِ الْمُؤْمِنِ، إِنَّ أَمْرَهُ كُلَّهُ خَيْرٌ- وَلَيْسَ ذَاكَ لِأَحَدٍ إِلَّا الْمُؤْمِنِ-، إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَّاءُ شَكَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَّاءُ صَبَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ"

**“jambo la Muumini ni jambo ajabu, kwani jambo lake lote ni la kheri -na hilo si la mtu yeyote ila Muumini- kama**

**akipata furaha hushukuru, na hilo ni kheri kwake, na akipata balaa husubiri na hilo ni kheri kwake.”**

Miongoni mwa matendo mazuri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kwamba Yeye (S.W) huleta faraja baada ya shida, na wepesi baada ya uzito na dhiki, ambpo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

"فَإِنَّ مَعَ العُسْرِ يُسْرًا * إِنَّ مَعَ العُسْرِ يُسْرًا"

**"Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi, Hakika pamoja na uzito upo wepesi",** Basi jambo likikuwa na shida, litakuwa na faraja, kwani shida haitakuja mara mbili badala ya faraja mmoja kamwe, na wala hakuna kitu baada ya shida isipokuwa faraja, wala hakuna kitu baada ya dhiki isipokuwa wepesi, ambapo Mtume wetu (S.A.W) anasema:

"وإن الْفَرَجَ مع الْكَرْبِ، وَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا"

**“Na Kwa hakika faraja huja pamoja na shida, na pamoja na shida huja wepesi”.**

Na mwenye kuzingatia katika maisha ya Mitume (rehma na amani ziwe juu yao) ataikuta maana hii dhahiri sana, mfano wa hayo ni bwana wetu Yaaqub (amani iwe juu yake) wakati alipopotea mwanawe aliyempendwa sana kwake, bwana wetu Yusuf (amani iwe juu yake), kisha akapotea mwanawe wa pili baada ya miaka michache, hadi alipoteza uwezo wa kuona kutokana na kilio na huzuni kwa kutenganishwa na wanawe wawili,

"وَابْيَضَّتْ عَيْنَاهُ مِنَ الْحُزْنِ فَهُوَ كَظِيمٌ"

**"Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni aliyo kuwa akiizuia",** ingawa hayo yote, basi yeye hakupoteza matumaini, ambapo Qur’ani Tukufu imesema juu ya ulimi wake:

"يـا بَنِـيَّ اذْهَبُـوا فَتَحَسَّسُـوا مِـنْ يُوسُـفَ وَأَخِيـهِ وَلا تَيْأَسُـوا مِـنْ رَوْحِ اللَّهِ إِنَّـهُ لا يَيْأَسُ مِنْ رَوْحِ اللَّهِ إِلا الْقَوْمُ الْكافِرُونَ"

**"Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa watu makafiri"** na anapata faraja kutoka kwa Mwenyezi Mungu (S.W) baada ya shida na balaa, Mwenyezi Mungu humrudishia uwezo wa kuona na watoto wake wawili, ambpo Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W) anasema:

"فَلَمَّا أَنْ جَاءَ الْبَشِيرُ أَلْقَاهُ عَلَى وَجْهِهِ فَارْتَدَّ بَصِـيرًا قَـالَ أَلَـمْ أَقُلْ لَكُـمْ إِنِّـي أَعْلَـمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ"

**"Basi alipo fika mbashiri na akaiweka kanzu usoni pake alirejea kuona. Akasema: Je! Sikukwambieni kuwa mimi najua ya Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi?"**

Mwenyezi Mungu amemuokoa Nabii Yunus (rehema na amani ziwe juu yake) kutokana na giza la bahari, usiku, na tumbo la nyangumi, basi shida imebadilishwa kwa faraja, na na dhiki imebadilishwa kwa wepesi, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W) anasema:

"وَذَا النُّونِ إِذْ ذَهَبَ مُغَاضِبًا فَظَنَّ أَلَّن نَّقْدِرَ عَلَيْـهِ فَنَـادَى فِـي الظُّلُمَـاتِ أَنْ لَا إِلَـهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِـنَ الظَّـالِمِينَ* فَاسْتَجَبْنَا لَـهُ وَنَجَّيْنَـاهُ مِـنَ الْغَمِّ وَكَذَلِكَ نُنْجِـي الْمُؤْمِنِينَ"

**"Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipo kuwa Wewe Subhanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu, Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo tunavyo waokoa Waumini"**

Na Mwenyezi Mungu anamruzuku bwana wetu Nabii Zakaria (amani iwe juu yake) kijana baada ya uzee wake, udhaifu wa mifupa na nyama, na kichwa ckake kimekuwa na nywele nyeupe, basi Mwenyezi Mungu akamjibu maombi yake wakati alpokuwa anamwomba na anatoa duaa.

"قَالَ رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ * فَنَادَتْهُ الْمَلَائِكَةُ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي الْمِحْرَابِ أَنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحْيَى مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَسَيِّدًا وَحَصُورًا وَنَبِيًّا مِنَ الصَّالِحِينَ."

**"Pale pale Zakariya akamwomba Mola wake Mlezi, akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka kwako uzao mwema. Wewe ndiye unaye sikia maombi, Alipo kuwa kasimama chumbani akisali, Malaika kamnadia: Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria Yahya, ataye kuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu, na ni bwana na mt'awa na Nabii kwa watu wema"**

Na mwenye kuzingatia katika matini ya sheria ya Kiislamu ataona kwamba Mwenyezi Mungu (S.W) ameifanya milango na funguo kwa faraja, miongoni mwa milango hayo ni: umuhimu wa uchamungu, na kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu kwa dua, na kumkumbuka, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W) anasema:

"وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا * وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا"

**"Na anaye mcha Mwenyezi Mungu humtengezea njia ya kutokea, Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia. Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake",** pia Mola Mtukufu anasema:

"أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ أَإِلَـهٌ مَّعَ اللَّهِ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ"

**"Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia"**

Na Mtume wetu (S.A.W) alikuwa anamwomba Mwenyezi Mungu kwa maneno hayo wakati wa dhiki:

"لا إلـهَ إلا اللهُ العظيمُ الحليمُ، لا إلـهَ إلا اللهُ ربُّ العرشِ العظيمِ، لا إلـهَ إلا اللهُ ربُّ السماواتِ وربُّ الأرض رب العرشِ الكريمِ"

**“Hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu, ndiye Mkuu, na Mpole, hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa Arshi kuu, hapana mungu ila Mwenyezi Mungu. Mola Mlezi wa mbingu na Mola Mlezi wa ardhi, Mola Mlezi wa Arshi tukufu"**

pia akasema (rehma na amani ziwe juu yake):

"من أصابَهُ همٌّ أو غمٌّ أو سقَمٌ أو شدَّةٌ فقالَ : اللهُ ربِّي لا شريكَ لـهُ . كُشِفَ ذلِكَ عنهُ"

**(Aliyepatwa na dhiki, huzuni, maradhi, au shida, na akasema: Mwenyezi Mungu ni Mola wangu, hana mshirika, basi kila mambo haya yataondoka kutokana naye).**

Ninaisema kauli yangu hii na ninamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu msamaha kwa ajili yangu na yenu.

Na tunazungumza katika hotuba yapili juu ya umuhimu wa kumtaja Mwenyezi Mungu na kumwomba msamaha na maghufira wakati wa shida na daraja.Ndugu zangu waislamu tunazungumza pia i juu ya **"kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wa shida na faraja"**

**الحمدلله رب العالمين والصلاة والسلام على أشرف المرسلين سيدنا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين، ثم أما بعد**

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu anaystahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu msalie, mpe salamu na umbariki yeye, Familia yake, Masahaba zake, na Kila atakayewafuata kwa wema mpaka Siku ya Malipo.

**Ndugu zangu Waislamu:**

Hakuna shaka kwamba hakuna kitu chochote ambacho ni nzuri zaidi kuliko na mtu anayedumisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu katika hali ya shida na faraja, hali ya dhiki na afya, na wala asiwe miongoni mwa wale ambao Qur'ani Tukufu ilituonya kutoka matendo yao, ambapo walisahau kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wa afya njema, na hawazikushukuru neema zake, ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema akituonya kutoka matendo yao:

"وَإِذَا مَسَّ الإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا خَوَّلَهُ نِعْمَةً مِنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ يَدْعُو إِلَيْهِ مِنْ قَبْلُ وَجَعَلَ لِلَّهِ أَنْدَادًا لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِهِ"

**"Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake",** pia anasema Mola Mtukufu:

"وَإِذَا مَسَّ النَّاسَ ضُرٌّ دَعَوْا رَبَّهُمْ مُنِيبِينَ إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا أَذَاقَهُمْ مِنْهُ رَحْمَةً إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ"،

**"Yakiwapata watu madhara humwomba Mola wao Mlezi nao wametubu kwake. Kisha akiwaonjesha rehema itokayo kwake, mara kikundi miongoni mwao humshirikisha Mola wao Mlezi",** Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema pia:

"وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ فَلَمَّا نَجَّاكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ الْإِنْسَانُ كَفُورًا"،

**"Na inapo kufikieni taabu katika bahari, hao mnao waomba wanapotea, isipo kuwa Yeye tu. Na anapo kuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha",** Mwenyezi Mungu anasema tena:

"وَإِذَا مَسَّ الإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنْبِهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَى ضُرٍّ مَّسَّهُ كَذَلِكَ زُيِّنَ لِلْمُسْرِفِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ"،

**"Na mtu akiguswa na shida hutuomba naye kaegesha ubavu, au kakaa, au kasimama. Lakini tukimwondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba tumwondoshee shida iliyo mpata. Ndio namna hiyo wamepambiwa warukao mipaka yale waliyo kuwa wakiyatenda",** pia anasema Mola Mtukufu:

"قُلْ مَن يُنَجِّيكُم مِّن ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً لَّئِنْ أَنجَانَا مِنْ هَذِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ"

**"Sema: Ni nani anaye kuokoeni katika giza la nchi kavu na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa siri, mkisema: Kama akituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanao shukuru",** aya hizi zinaonyesha hali za wanaomuomba Mwenyezi Mungu wakati wa shida na dhiki tu, basi kama Ikiwa Mwenyezi Mungu amewaondolea shida na dhiki, wanarudi tena kwenye hali zao mbaya.

Bila shaka, sisi sote tunahitaji kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya neema zake, wakati wa faraja, subira wakati wa mitihani na dhiki, na kudumisha kumkumbuka yeye (S.W) wakati wa furaha  na shida, amababapo Mtume wetu (S.A.W) anasema:

"مَنْ سَرَّهُ أَنْ يَسْتَجِيبَ اللهُ لَهُ عِنْدَ الشَّدَائِدِ وَالكَرْبِ، فَلْيُكْثِرِ الدُّعَاءَ فِي الرَّخَاءِ"

**" Mtu yeyote anayetaka Mwenyezi Mungu amjibu wakati wa shida na dhiki, basi aombe dua nyingi Mwenyezi Mungu wakati wa faraja",** na anasema (rehma na amani ziwe juu yake):

"تَعرَّفْ إلى اللهِ في الرخاءِ يعرفُك في الشدَّةِ"

**"ujue Mwenyezi Mungu wakati wa faraja, naye atakujua wakati wa dhiki"**

Bwana wetu Abu al-Dardaa' (radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake) anasema:

"ادع الله يوم سرَّائك يستجب لك يوم ضرَّائك"

**"Muombie Mwenyezi Mungu siku ya faraja yako, naye atakujibu siku ya shida yako".**

Ewe Mwenyezi Mungu, mwondoshee huzuni kila mwenye huzuni, na uturuzuku tuwe ni wenye kukushukuru kwa neema na baraka zako (kwetu)

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuumba uilinde nchi yetu pamoja na nchi yote za Kiislamu na misho wa Dua yetu ni Alhamdulillahi Rabilaalameena

والسلام عليكم ورحمة الله وبركاته